**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

Simu: +255262963470
Barua pepe: ps@mit.go.tz
Barua pepe: gcu@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz
Faksi +255262963117

Mji wa Serikali
Mtumba,
Mtaa waViwanda,
S.L.P 2996,
**40478 DODOMA,**

## TAARIFA KWA UMMA

---

## MWENENDO WA BEI YA BIDHAA MUHIMU NCHINI

**11/04/2022, DAR ES SALAAM.**

Mtakumbuka takriban mwezi mmoja uliopita nilizungumza na umma kupitia kwenu Waandishi wa Habari kuelezea mwenendo wa kupanda kwa bei mbalimbali katika soko letu na kueleza kuwa Serikali inafuatilia suala hili kwa karibu na kwa umakini mkubwa na niliahidi kuwa uchunguzi wa kina utakapokamilika nitawaeleza nini tulichokibaini. Aidha nilielekeza mamlaka zinazohusika katika **kusimamia mwenendo wa soko la bidhaa** kuchukua hatua za kisheria pale ambapo chanzo cha kupanda bei itathibitika kuwa ni michezo ya wafanyabiashara. Hapa nilielekeza Tume ya Ushindani ambayo kisheria ina jukumu la kulinda maslahi ya wadau katika soko kutimiza wajibu huo.

Aidha, baada ya taarifa yangu kwa Umma, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia kwa Katibu Mkuu ilitoa ufafanuzi kwa umma kwamba Sheria ya Ushindani ndiyo sheria mama inayotumika kudhibiti vitendo vya kuvuruga **mwenendo we** bei sokoni. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 9 (1) cha Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003 (Fair Competition Act, No. 8 of 2003) kinachozuia makubaliano ambayo malengo, matokeo au matokeo tarajiwa yake ni washindani:
(a) kupanga bei,
(b) kufanya mgomo,
(c) kukubaliana katika manunuzi, na
(d) kuzuia uzalishaji.

Pamoja na juhudi hizi za Wizara yangu, Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza pia kuundwa kwa jopo lingine la wataalamu kufuatilia mwenendo wa bei. Hivyo, katika eneo hili tunaweza kusema kwamba, Serikali imechukulia suala la kupanda kwa bei za bidhaa kwa uzito mkubwa sana na hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Kwa muktadha huu, leo nimekuja mbele yenu kutoa matokeo ya tathmini iliyofanywa katika kufuatilia mwenendo wa mabadiliko ya bei **za baadhi ya bidhaa** katika soko letu la ndani. Katika kufanya tathmini hii mambo ya msingi yaliyozingatiwa ni;

- Kuangalia kama kulikuwa na mabadiliko ya bei baada ya ufuatiliaji na yale tuliyoyabaini katika hatua za awali tulipopeana taarifa,
- Ukweli juu ya mabadiliko ya bei katika soko la dunia kutokana na athari ya janga la UVIKO-19 na kwa namna gani yanaathiri mwenendo wa bei hapa nchini,
- Ni kwa kiwango gani sababu za ndani ya nchi hasa vitendo vya wafanyabiashara ambao si waaminifu hupandisha bei baaada tu ya kusikia kuwa bei katika soko la dunia zinabadilika, na
- Aidha kufuatia mgogoro wa Urusi na Ukraine tathmini iliongeza jukumu hili.

**Nini matokeo ya tathmini ya mwenendo wa bei?**

Tathmini ya kina iliyofanyika imeonesha kwamba bei ya bidhaa nyingi zinazozalishwa nchini bei zake zina uhimilivu mkubwa (stable) na pia zipo bidhaa chache kama saruji na nondo ambazo bei zake zilikuwa zimepanda kwa viwango visivyohimilika. Aidha, kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi tathmini imeonyesha kuwa na bei zisizo na utulivu na zisizohimilika.

Tathmini pia imeonyesha kuwepo kwa visababishi vya upandaji wa bei ya bidhaa hizo ikiwa ni pamoja na:

(i) Uwepo wa janga la UVIKO-19 lililosababisha chumi nyingi kufungwa kama moja ya njia ya kukabiliana na ugonjwa huu na hivyo kuzuia bidhaa na rasimali kuhama kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine;

(ii) Upungufu wa bidhaa mbalimbali katika soko la dunia kutokana na kusimama kwa uzalishaji viwandani;

(iii) Kuongezeka kwa gharama za usafirishaji kunakotokana na ukosefu wa makasha ya kubebea bidhaa (kontena);

(iv) Mgogoro kati ya Urusi na Ukraine pia umeonekana kuathiri mwenenedo wa bei ya baadhi ya bidhaa duniani ikiwemo Tanzania.

**Hali Ikoje ya baadhi ya bei za bidhaa baada ya Taarifa yetu ya mwisho?**

**Kutokana na tathmini na uchambuzi wa kina uliofanywa**, bei za baadhi ya bidhaa nchini hasa saruji na sukari zimeonesha kupungua kidogo tofauti na ilivyotegemewa hasa baada ya kupungua kwa changamoto za UVIKO-19. Kama tunavyojua mwenendo wa bei ya saruji haukuwa tulivu kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 na hivyo bei ilipanda hadi kufikia wastani wa shilingi 17,700 mwezi Februari 2022. Hata hivyo, baada ya jitihada mbalimbali za Serikali ikiwemo kuongea

na wazalishaji wa saruji hatimaye bei imeanza kupungua hadi kufikia wastani wa shilingi 16,125 mwezi Machi, 2022.

Hata hivyo, bei hizo zinatakiwa kuendelea kushuka zaidi ukizingatia bei halisi ya uzalishaji na usafirishaji haziakisi bei za bidhaa husika sokoni. **Mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali na Wadau muhimu katika sekta hii na tathmini ya kina inaendelea kufanyika kwani kuna hoja kwamba ongezeko kubwa la bei za bidhaa hizi hutokea mara tu bidhaa zitokapo nje ya kiwanda.** Natoa wito kwa wazalishaji wa saruji nchini kuhakikisha makubaliano yetu yanatekelezwa kama yalivyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanaondoa urasimu wa utoaji wa saruji viwandani. Wizara yetu itaendelea kusimamia kwa upande wa wasambazaji na wauzaji wa rejareja ili kuhakikisha hawaongezi bei bila sababu za msingi.

**Athari za Vita kati ya Urusi na Ukraine.**

Bidhaa zenye mfungamano wa moja kwa moja na mgogoro kati ya Urusi na Ukraine ni kama vile Ngano, Mafuta ya kula, Mbolea, mafuta ya Petroli, Dizeli na mafuta ya Taa.

***a) Ngano***

Tukianza na bidhaa ya ngano, Nchi za kiafrika zinaagiza ngano kwa wingi kutoka Urusi na Ukraine kila mwaka inayokadiriwa kufikia dola za kimarekani bilioni 4. Mnufaika mkubwa katika uagizaji huu ni Misri ikufuatiwa na Sudan, Nigeria, Tanzania, Algeria, Kenya na Afrika ya Kusini. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2021 Tanzania ilikuwa nchi ya 53 inayoagiza ngano kwa wingi duniani na kati ya ngano hiyo asilimia 57 ilitoka Urusi na Ukraine; Urusi ikichangia sehemu kubwa. Kwa wastani Tanzania inaagiza na kuingiza nchini Ngano 800,000MT, huku uwezo wetu wa kuzalisha ngano ndani ya nchi ikiwa ni wastani wa 100,000 MT kwa mwaka. Hivyo tunaweza kuona ni kwa kiasi gani vita kati ya Nchi mbili hizi ilivyo na athari za moja kwa moja kwenye bei ya ngano ndani ya Taifa letu.

***b) Mafuta ya Kula***

Mafuta ya kula nayo yamekumbwa na athari kubwa kutokana na vita ya Urusi na Ukraine. Mapema mwaka 2019 kabla ya janga la UVIKO-19 bei ya mafuta ya kula yalikuwa dola za kimarekani 700 kwa tani moja ya mafuta, huku wakati wa janga la UVIKO-19 bei yake ikaongezeka hadi kufikia dola za kimarekani 1,760 kwa tani moja ya mafuta ya kula kwa mwaka 2020/21. Baada ya kuanza kwa vita ya Urusi na Ukraine, Dunia imeshuhudia bei ya mafuta ya kula ikipanda kutoka Dola za Kimarekani 1760 kwa tani moja mwaka 2020/21 hadi kufikia Dola za kimarekani 1980 kwa tani moja mwaka 2022.

Ongezeko hili la bei ya mafuta Duniani lina athari hasi kubwa kwetu Watanzania, kwani uhitaji wa mafuta ndani ya Taifa letu kwa mwaka ni tani 650,000 (MT) huku uwezo wetu wa kuzalisha mafuta ni tani 270,000 (MT) ambayo ni sawa na asilimia

41.5 tu ya mahitaji yetu kwa mwaka. Maana yake ni kwamba ongezeko lolote la bei ya mafuta ya kula kwenye soko la Dunia lina athari hasi za moja kwa moja na bei ya bidhaa hiyo kwenye soko letu la ndani.

*c). Mbolea*

Mbolea ni moja ya bidhaa ambayo nayo imeathirika sana na janga la UVIKO-19 pamoja na Vita ya Urusi na Ukraine. Kwa mfano, katika mwaka 2019 kabla ya janga la UVIKO-19 bei ya mbolea katika Soko la Dunia kwa tani moja ilikuwa ni Dola za Marekani **396** (Mbolea aina ya DAP) na Dola za Marekani **249** (Mbolea aina ya UREA) ikilinganishwa na mwaka 2021 wakati wa janga la UVIKO-19 ambao bei ya mbolea hizo zilipanda hadi kufikia Dola za Marekani **551** (Mbolea aina ya DAP) na Dola za Marekani **362** (Mbolea aina ya UREA). Aidha, hadi kufikia mwezi Machi, 2022 ambapo vita kati ya Urusi na Ukraine vikiendelea bei za mbolea hizo zimepanda hadi kufikia Dola za Marekani **1012** (DAP) na Dola za Marekani **1214** (UREA).

Ongezeko hili la bei ya mbolea Duniani lina athari hasi kubwa kwetu Watanzania, kwani uhitaji wa mbolea ndani ya Taifa letu kwa mwaka ni Tani **700,000** ikilinganishwa na uwezo wetu wa kuzalisha mbolea ni Tani **30,000** kwa mwaka. Maana yake ni kwamba ongezeko lolote la bei ya mbolea kwenye soko la Dunia lina athari hasi za moja kwa moja kwenye bei ya bidhaa hiyo kwenye soko letu la ndani. Ndiyo maana mwaka 2019 bei ya mfuko mmoja wa Kg 50 wa mbolea aina ya DAP uliuzwa kwa shilingi **57,886** na UREA uliuzwa kwa shilingi **52,000**, huku mwaka 2021 uliuzwa kwa shilingi **66,995** (DAP) na shilingi **55,869** (UREA) na hatimaye mwaka 2022 baada ya kuanza kwa vita vya Urusi na Ukraine tumeshuhudia mfuko mmoja wa mbolea ya DAP ukiuzwa kwa shilingi **110,000** (DAP) na shilingi **104,000** (UREA). Hii ina maana kubwa sana kwani Nchi za Urusi na Ukraine ni wazalishaji na wasambazaji mkubwa wa bidhaa ya mbolea kwa gharama nafuu Duniani ikilinganishwa na nchi nyingine. Tanzania imekuwa ikiagiza kiasi kikubwa cha mbolea kutoka katika nchi za Urusi na Ukraine. Kwa mfano, katika Msimu wa kilimo wa 2019/20 TFRA ilitoa vibali vya kuagiza jumla ya **Tani 17,376** za mbolea kutoka nchini Urusi na **Tani 75,947** kutoka nchini Ukraine; Msimu wa kilimo wa 2020/21 TFRA ilitoa vibali vya kuagiza jumla ya **Tani 64,117** za mbolea kutoka nchini Urusi; na Msimu wa Kilimo 2021/22 unaoendelea hadi kufikia mwishini mwa mwezi Februari, 2022 TFRA imeshatoa vibali vya kuagiza jumla ya **Tani 34,400** za mbolea aina ya NPK na UREA kutoka nchini Urusi.

*d). Mafuta ya Petroli, Dizeli na Taa (Nishati).*

Mafuta ya Petroli, Dizeli na mafuta ya Taa ni moja ya bidhaa ambazo nazo zimeathirika sana na janga la UVIKO-19 pamoja na Vita ya Urusi na Ukraine. Mwaka 2019 kabla ya janga la UVIKO-19 mfano bei ya mafuta ya Petroli katika Soko la Dunia ilikuwa ni wastani wa Dola za Marekani **594.82** kwa tani moja ya Petroli; huku wakati wa janga la UVIKO-19 mwaka 2021 bei ya Tani moja ya Petroli ilikuwa ni wastani wa Dola za Marekani **671.04.** Aidha, baada ya kuanza kwa vita ya Urusi na Ukraine kuanzia mwezi Januari hadi Machi, 2022 bei ya Tani moja ya Petroli ni wastani wa Dola za Marekani **942.13**.

Kwa upande wa Mafuta ya Dizeli, bei katika soko la dunia mnamo mwaka 2019 kabla ya UVIKO-19 ilikuwa ni wastani wa Dola za Marekani **576.20** Kwa tani moja ikilinganishwa na kipindi cha UVIKO-19 mwaka 2021 ambapo bei zilishuka kidogo hadi kifikia wastani wa Dola za Marekani **574.71** kwa tani moja. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 ambapo vita kati ya Urusi na Ukraine vinaendelea bei ya bidhaa hiyo ilipanda maradufu hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani **881.88** kwa tani moja.

Bei ya Mafuta ya Taa katika soko la dunia mwaka 2019 kabla ya UVIKO-19 ilikuwa ni wastani wa Dola za Marekani **594.94** kwa tani moja ikilinganishwa na mwaka 2021 kipindi cha UVIKO-19 ambapo bei ilikuwa ni wastani wa Dola za Marekani **580.35** kwa tani moja. Aidha, bei ya bidhaa hiyo ilipanda hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani **868.26** kwa tani kwa kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 ambapo vita kati ya Urusi na Ukraine vinaendelea.

Kupanda kwa bei ya bidhaa hizi kuna athari ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja na bei za bidhaa na huduma nyingine. Mfano, unakuta mtu anauliza kwanini vita ya Urusi na Ukraine inasababisha bei ya Kokoto au Mchanga kupanda. Jibu lake ni rahisi tu Mchanga au Kokoto vinasafirishwa kwenye magari yanayotumia mafuta ambayo yamepanda bei, hivyo ili mtoa huduma hii aweze kuendelea na biashara yake lazima ataongeza bei ya mchanga au kokoto kufidia gharama za mafuta zilizoongezeka. Sote tunatambua ongezeko japo kidogo kwenye nishati yoyote iwe umeme au mafuta ina athari kubwa kwenye mnyororo mzima wa utoaji wa huduma na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwenye viwanda vyetu na hatimaye kwenye ufikishaji wa bidhaa hizo kwa Wananchi.

**HALI ILIVYO KWENYE NCHI ZA AFRIKA MASHARIKI.**

Tathmini pia iliangalia mwenendo wa bei za bidhaa hizi katika nchi zaukanda wa Afrika Mashariki; na matokeo yakaonyesha kuwa nchi za kenya, Uganda, Rwanda na Burundi zimekumbwa na mwenendo uleule wa ongezeko la bei za baadhi ya bidhaa muhimu. Wastani wa bei kwa bidhaa zote katika nchi hizo kwa Mwezi machi 2022 uko juu kuliko Tanzania isipokuwa mafuta ya kula.

**Mfano**:

(i) Wastani wa bei ya saruji (50kg) kwa nchi za Afrika Mashariki ni TSH. 16,527 ikilinganishwa na TSH. 16,125 kwa Tanzania.

(ii) Wastani wa bei ya petrol (lita 1) kwa nchi za Afrika Mashariki ni TSH. 2,971 ikilinganishwa na TSH. 2,616 kwa Tanzania.

(iii) Wastani wa bei ya Gesi ya kupikia (6 kg) kwa nchi za Afrika Mashariki ni TSH. 33,454 ikilinganishwa na TSH. 23,000 kwa Tanzania.

(iv) Wastani wa bei ya mafuta ya kula (lita 1) kwa nchi za Afrika Mashariki ni TSH. 7,470 ikilinganishwa na TSH. 7,625 kwa Tanzania.

(v) Wastani wa bei ya unga wa ngano (kilo 1) kwa nchi za Afrika Mashariki ni TSH. 1,886 ikilinganishwa na TSH. 1,735 kwa Tanzania.

(vi) Wastani wa bei ya sukari (kilo 1) kwa nchi za kwa nchi za Afrika Mashariki ni TSH. 3,034 ikilinganishwa na TSH. 2,672 kwa Tanzania.

(vii) Wastani wa bei ya bati (geji 30) za kwa nchi za Afrika Mashariki ni TSH. 24,978 ikilinganishwa na TSH. 21,952 kwa Tanzania

(viii) Wastani wa bei ya nondo (12mm) kwa nchi za Afrika Mashariki ni TSH. 42,113 ikilinganishwa na TSH. 25,911 kwa Tanzania

**Mikakati ya muda mfupi**

Kutokana na tathmini pamoja na taarifa hii ninayoitoa mbele yenu, Serikali imeendelea na itaendelea kuchukua hatua zifuatazo ili kudhibiti upandaji holela wa bei za bidhaa mbalimbali kwenye soko letu la ndani;

a) Mamlaka na Taasisi za Serikali zilizopewa dhamana ya kusimamia mienendo ya masoko ya bidhaa zitaendelea kutekeleza wajibu huo kikamilifu na kwa umakini mkubwa ili kudhibiti vitendo vya upandishaji holela wa bei za bidhaa nchini hasa bidhaa zote zinazozalishwa Nchini;

b) Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara itaendelea kufanya vikao kazi na wadau wote muhimu kwenye eneo la Viwanda na Biashara ili kuhakikika mgutuko wa Uchumi wa ndani unatafutiwa majibu ya haraka. Mf. Bei ya sukari, saruji, nondo, vinywaji baridi na baadhi ya vyakula -- bei zimepungua na ni himilivu kwa sasa.

c) Serikali kupitia WUVB imeanzisha mfumo wa upatikanaji wa bei za bidhaa mbalimbali kila siku, pia kutakuwa na call Centre itakayotumika kupokea simu kutoka kwa Wananchi kuhusu mienendo isiyoridhisha ya bei za bidhaa sokoni;

d) Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za muda mfupi kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kula nchini ikiwa ni pamoja na: Kutoa Motisha kwa Waagizaji (Exporters) wa Mafuta ya Alizeti; Kutoa mikataba ya utekelezaji (Perforamance Agreement) kwa Wachakataji wa zao la chikichi; Kutoa motisha za kikodi (Tax incentives) kwa waagizaji wa mafuta ya kula; Kusambaza mbegu bora za Alizeti kwa wakulima; 2022 tani 2000 za alizeti zimesambazwa, huku kwa mwaka 2023 tani 5000 za begu bora za alizeti zitasambazwa kwa wakulima;

e) Kuimarisha huduma za ugani nchini kwa kuhakikisha kuwa Maafisa Ugani wanawafikia Wakulima na kutoa huduma stahiki kwa wakati. Katika kutimiza azma hiyo Serikali imegawa pikipiki 6,704 kwa Maafisa Ugani nchini kote, na

f) Maafisa Biashara wa Mikoa yote nchini wataendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa mbalimbali kwenye maeneo yao na kuwasilisha taarifa hizo mara kwa mara Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa, ili itakapobidi hatua stahiki zichukuliwe kwa wakati;

**Mikakati ya muda mrefu**

Katika kukabiliana na changamoto za kupanda kwa bei za bidhaa, Serikali ina mikakati ya muda mrefu ikiwa ni pamoja na:

a) Kuendelea kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika viwanda muhimu ili kuzalisha bidhaa muhimu kwa kukidhi mahitaji ya ndani na kwa ufanisi ili kupunguza gharama za uzalishaji. Maeneo muhimu ya uwekezaji huo ni katika

uzalisaji wa bidhaa za chakula zinazoingizwa kwa wingi kutoka nje ikiwemo Ngano, Mafuta ya Kula na Sukari ikiwemo kujenga ngazi tatu za Viwanda vya Alizeti nchini ili kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kula.

b) Kuwezesha upatikanaji wa pembejeo muhimu za kilimo ikiwa ni pamoja na kuhamasisha na kuvutia uwekezaji wa ujenzi wa viwanda vya ndani vya kuzalisha mbolea ikiwemo uanzishwaji wa Kiwanda kipya cha INTRACOM kilichopo Nala, Dodoma ambapo uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2022 ambapo Tani 600,000 za mbolea zinatarajiwa kuzalishwa kwa mwaka katika kiwanda hicho; Kuhimiza viwanda vilivyopo kuongeza uzalishaji wa mbolea; na Kufufua mradi wa uzalishaji wa mbolea za UREA na CAN kwa kutumia Gesi asilia.

c) Katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa Sukari nchini, Serikali ya awamu ya 6 inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji mpya katika viwanda vya kuzalisha sukari. Katika kuthibitisha jambo hili tunaona uwekezaji mkubwa kwenye viwanda vya sukari vya Mtibwa na Kagera wenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa hii. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na wawekezaji wapya ambao wameonesha nia ya kuwekeza katika eneo la uwekezaji la Mkulazi; Uwekezaji huo unakadiriwa kufikia **TZS Bilioni 344** pamoja na Mradi wa Bagamoyo Sugar unaokadiriwa kufikia **Dola za Marekani Milioni 198**.

**NINI TUNAJIFUNZA**

Changamoto za kijamii na kiuchumi zina athari mtambuka haijalishi changamoto hiyo imetokea upande gani wa Dunia. Ulimwenguni umekumbwa na tatizo la mfumko mkubwa wa bei hali ambayo inaweza kupelekea Dunia kuingia kwenye mdororo wa Uchumi kama tuliouona mwaka 2008. Hata hivyo imejidhihirisha wazi kwamba Uwekezaji wa ndani kwenye uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbili ni muhimu sana katika kuhimili mtikisiko wowote wa Kiuchumi Duniani. Hivyo basi kama kauli mbiu ya Mpango wa tatu wa maendeleo inavyosema "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu"; mtikisiko huu ni fursa kwetu Watanzania hasa Wawekezaji wa ndani na pia wa nje kuja kuwekeza kwenye maeneo haya ili kupunguza athari za mabadiliko yoyote ambayo yanaweza kutokea Duniani. Mhe.Samia Suluhu Hassan ameiona fursa hii na ndiyo maana anaendelea kuvutia wawekezaji wote wa ndani na nje waje kuwekeza ndani ya Taifa letu.

Wito wangu kwa Wawekezaji na wafanyabiashara wetu wa ndani waitumie fursa hii kimkakati kabisa, na waweze kuwapokea Wawekezaji na Wafanyabiashara wetu wa nje wanaokuja kuwekeza ndani ya Taifa letu ili tusafiri pamoja katika safari hii ya maendeleo.

**HITIMISHO**

Ndugu Waandishi wa Habari, Kama ilivyo kawaida yangu, napenda kuhitimisha taarifa yangu kwa kuweka wazi; kuwa mwelekeo wa sera za Uchumi wa kuachia nguvu za soko huria katika uendeshaji wa biashara, ikiwa ni pamoja na Serikali kuachana na jukumu la kupanga bei, hauna maana ya kuondoa jukumu la msingi la Serikali la kusimamia ushindani wa haki kwenye soko. Sisi kama Serikali tuna wajibu wa kudhibiti mienendo hadaifu au kandamizi ya wazalishaji wa bidhaa na wafanyabiashara kwenye soko ikiwa ni pamoja na upandishaji holela wa bei.

Hivyo basi, Serikali ya CCM inayoongozwa na Mwana Mama mahiri Mhe.Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitavumilia tabia ya wafanyabiashara wachache kuanzia wazalishaji hadi wasambazaji wenye dhamira ovu ya kuwaumiza wananchi kwa kujiamulia kupandisha bei za bidhaa bila kufuata utaratibu kwa manufaa yao binafsi. Serikali Inawaelekeza wazalishaji na Wasambazaji wa bidhaa muhimu kuweka bei zinazoendana na uhalisia wa soko ikiwa ni pamoja na kutotumia kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhan na Kwaresma kubandisha bei.

11/04/2022

**Dkt. Ashatu Kijaji (Mb)**
**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**